# GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

*(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)*

Sehemu ya CXXV Nam. 6656 — 16 Juni, 2017 — Bei Shs. 5,000/=

*Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti* — *Hutolewa kila Ijumaa*


YALIYOMO — *Ukurasa*


Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa nam. 7 ya 2014
Kanuni za huduma zinazotolewa na
Mamlaka za Serikali za mitaa
(Chini ya Kifungu cha 94). .................................................... 85

Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa nam. 7 ya 2014
Kanuni za Usuluhishi wa Migogoro
(Chini ya kifungu cha 94). ............................................. 112


SEHEMU YA SHERIA

Tangazo la Sheria lililotajwa hapo chini limetangazwa katika *Gazeti Rasmi* hili

Tangazo la Sheria

Nam. 63 :- Kanuni za Mamlaka za Serikali za Mitaa.
64 :- Kanunu za Usuluhishi wa Migogoro.

## SHERIA YA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MTAA NAM. 7 YA 2014

## KANUNI ZA HUDUMA ZINAZOTOLEWA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA.

### MPANGILIO WA KANUNI

KANUNI — MAELEZO

SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Tafsiri.


Matangazo yaliyohusu maiti, kuvunjika kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanaweza kutiwa katika Gazeti. Nakala matangazo namna hiyo, zipelekwe kwa Mhariri wa Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania katika nyumba ya kupiga Chapa, Sanduku la Posta 261. Nakala zisichelewe kuliko Jumatatu kila wiki.


Scanned with CamScanner

## SEHEMU YA PILI
## UHIFADHI WA MAZINGIRA NA UKUSANYAJI WA TAKA

3. Usafi wa Mazingira.
4. Marufuku kutupa taka.
5. Mamlaka itaridhika wajibu wa ukusanyaji na utupaji taka.
6. Ada ya usafi.
7. Majivu ya moto, taka za maji maji.
8. Utupaji taka baharini.
9. Utupaji taka na maji taka katika mitaro.
10. Uchimbaji wa karo na vyoo.
11. Serikali ya Mtaa inaweza kuweka vyombo vya kutilia taka.
12. Wajibu wa kufunika vyombo vya kuweka taka.
13. Kuchakura na kutawanya taka zilizokusanywa.
14. Uharibifu wa vyombo vya kuhifadhia taka.
15. Uhifadhi wa Masalia ya vyombo vya moto, umeme, magari ya ng'ombe na marikwama.
16. Kutupa taka, majitaka sehemu isioruhusika.
17. Mmiliki kusafisha eneo linalomzunguka.
18. Utupaji taka kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuombwa.
19. Kuondoa taka kwa kuombwa.
20. Vitu visivofaa kutupwa mitaani.
21. Taka za vigae.
22. Taka za vitu chakavu.
23. Adhabu.
24. Uchimbaji wa mchanga.
25. Marufuku kuchimba mtaani.
26. Uchimbaji, uchongaji wa matofali ya mawe, fusi na kokoto.
27. Udhibiti wa vyombo vya moto na magari katika maeneo ya mji.
28. Marufuku kwa vyombo na wanyama kupita kwenye njia za wenda kwa miguu.
29. Sehemu za hatari kuwekwa salama.
30. Adhabu.

## SEHEMU YA TATU
## UTARATIBU WA UTOWAJI WA LESENI ZA BIASHARA

31. Ukataji wa leseni.
32. Malipo ya leseni.
33. Biashara za kwenye magari mikokoteni na vyombo vya maringi mawili.
34. Ada ya biashara ndogo ndogo.
35. Kusitishwa kwa leseni ya biashara.
36. Kufuta leseni ya biashara.
37. Kupotea kwa leseni.
38. Utaratibu wa Ukaguzi wa maeneo ya biashara.
39. Afisa kubadili kiwango cha leseni.
40. Adhabu.
41. Marufuku kufunya biashara Mtaani.
42. Bidhaa kuacha kwa muda mrefu katika mitaa.
43. Kunin'giniza bidhaa Mtaani.
44. Leseni za wanyama.
45. Leseni ya gari linalokokotwa na mnyama, Binadamu au kusambazwa na gari.
46. Tangazo la biashara.
47. Matangazo ya Kampuni.
48. Ada ya mnada.

## SEHEMU YA NNE
## HUDUMA ZA USAFIRI

49. Vituo vya Daladala.
50. Utambulisho wa ruhusa ya njia.

51. Utoaji na matumizi ya beji.
52. Uwekaji wa Alama za rangi kwa gari za abiria.
53. Ada ya kuhaulisha Ardhi.
54. Ada ya Ujenzi.
55. Uwekeaji wa miundombinu.
56. Adhabu ya jumla.

## SEHEMU YA TANO
## UDHIBITI WA MAZAO YA MISITU NA MALIASILI

57. Ada ya mazao ya misitu.
58. Ada ya mazao ya Maliasili.
59. Ada ya kusafirisha mazao ya baharini.
60. Ada ya kukodisha mikarafuu.

## SEHEMU YA SITA
## ADA ZITOKANAZO NA KODI AU PANGO

61. Taarifa ya kukodisha mali zinazohamishika na zisizohamishika.
62. Mkodishaji wa ardhi kwa ujenzi wa mnara.
63. Ada ya ujenzi mnara na uendeshaji.
64. Ada za Uwekezaji kitega Uchumi.
65. Ada ya diko.
66. Usajili wa vyombo vya usafiri.
67. Mamlaka ya Serikali ya Mtaa kuweka uwekaji wa kumbukumbu.

## SEHEMU YA SABA
## UDHIBITI WA UZURURAJI WA WANYAMA

68. Ruhusa ya kufuga wanyama.
69. Uwezo wa kukamata mnyama.
70. Kuwapitisha na kufunga wanyama sehemu zisizoruhusika.
71. Kumfanyisha kazi mtoto chini ya umri wa miaka kumi na nane.
72. Kumtesa mnyama.
73. Utaratibu wa myama aliekamatwa.
74. Kuwapatia wanyama chanjo.
75. Maeneo ya majosho.

## SEHEMU YA NANE
## MAEGESHO YA VYOMBO VYA MOTO

76. Kuegesha na kupakia
77. Malipo ya kuegesha chombo.
78. Malipo ya kawaida na yale ya ziada.
79. Kuegesha chombo bila ya malipo.
80. Kusamehewa kufanya malipo.
81. Makosa.
82. Adhabu
83. Uwezo wa kuingia katika eneo.
84. Kushindwa kutii notisi.
85. Utumiaji wa Notisi.
86. Adhabu.
87. Jadweli la malipo ya ada za huduma
88. Kufutwa.

Scanned with CamScanner

Tangazo Nam. 34.

SHERIA YA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MTAA
NAM. 7 YA 2014

KANUNI ZAHUDUMA ZINAZOTOLEWA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA.
**(Chini ya kifungu cha 94)**

KWA UWEZO niliopewa chini ya kifungu cha 94 cha Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Nam.7 ya 2014, **Mimi HAJI OMAR KHERI** Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, natunga kanuni zifuatazo:

**SEHEMU YA KWANZA**
**UTANGULIZI**

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Kanuni hizi zitajulikana kama kanuni za Huduma zinazotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa za mwaka 2017 na zitaanza kutumika baada ya kutiwa saini na Waziri na kutangazwa kwenye Gazeti Rasmi la Serikali.

Tafsiri.

2. Katika Kanuni hii, isipokuwa kama maelezo yatahitajika vyenginevyo:

"Ada" maana yake ni pesa inayotozwa kwa ajili ya kupewa huduma katika eneo la Mamlaka za Serikali ya Mitaa;

"Afisa" maana yake ni mtumishi yeyote ambae ameajiriwa kwa ajili ya kufanyakazi za Mamlaka ya Serikali ya Mtaa;

"Afisa aliyeidhinishwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Mamlaka alieidhinishwa kufanya kazi za Mamlaka ya Serikali ya Mtaa;

"Beji" maana yake ni kitambulisho cha kazi kinachotolewa na taasisi inayotambulika na kutambuliwa na serikali;

"Biashara ndogo ndogo" maana yake ni biashara zote zinazofanyika ndani ya eneo la Mamlaka ya Serikali ya Mtaa ambazo hazihitaji leseni katika maeneo yaliyoruhusiwa kisheria;

"Gari" maana yake inajumuisha gari linalokokotwa na mnyama, linalotumia mashine au rikwama;

"Kibali" maana yake ni ruhusa iliyotolewa na Mamlaka ya Serikali za Mtaa kwa ajili ya kazi maalum;

"Maeneo ya Wazi"inajumuisha sehemu yoyote iliokuwa haimilikiwi na mtu au taasisi yeyote, iliyotengwa kwa ajili ya matumizi ya jamii au haija pangiwa matumizi na Serikali;

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Seikali za Mitaa;

Scanned with CamScanner

"Maliasili zisizorejesheka" maana yake inajumuisha mawe, kokoto, mchanga, udongo, matofali ya kuchonga kifusi na maliasili zinazofanana na hizo;

"Mkaguzi" maana yake mtu aliyeajiriwa kufanya kazi Mamlaka ya Serikali ya Mtaa na mwenye idhini ya kufanya ukaguzi katika Mamlaka hiyo;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali ya Mtaa alieteuliwa kwa mujibu wa kifungu cha 39 cha Sheria Namba 7 ya 2014;

"Mnada" maana yake ni biashara inayofanyika hadharani kwa utaratibu wa ushindani wa bei;

"Mnara" maana yake ni chombo kilichojengwa kwa madhumuni ya kupokea au kurejesha mawasiliano ya habari;

"Mtu" maana yake inajumuisha mtu binafsi, shirika, kampuni au Taasisi;

"Mvunaji wa mazao ya misitu" maana yake inajumuisha mkataji wa mti, kuni, mpigaji tanu ya chokaa au mkaa, mvunaji nta, asali na muwindaji wa wanyama;

"Njia za Miguu" inajumuisha chochoro pembeni mwa mtaa au sehemu yoyote ya mtaa iliojengwa au kuwekwa kwa ajili ya matumizi ya wapita kwa miguuna inajumuisha upenu kwa ajili ya uchukuzi;

"Stika" maana yake ni kitambulisho cha ruhusa ya njia kwa gari itakayofanya kazi katika eneo la Mamlaka ya Serikali ya Mtaa;

"Sehemu za Mjumuiko wa watu"inajumuisha soko au sehemu za burudani zilizomo ndani ya eneo la Mamlaka za Serikali za Mitaa;

"Tangazo la biashara" maana yake ni jina, alama au ujumbe unaoashiria uwepo wa kitu kinachouzwa au huduma inayotolewa katika eneo la Mamlaka;

"Vitu chakavu" maana yake ni vitu vyote vinavyotokana na mali zilizotumika ndani au nje ya nchi vyenye asili ya aluminium, plastiki, au chuma kama vile magari, friji ,friza, maredio, televisheni,vyombo vya matumizi ya nyumbani na vitu vyengine vinavyofanana navyo;

"Vyombo" maana yake inajumuisha vyombo vyote vya usafiri wa barabarani;

"Wanyama" maana yake ni wanyama wote ikijumuisha wanaofugwa na wasiofugwa ambao wamo katika eneo la Mamlaka ya Serikali ya Mtaa;

Scanned with CamScanner

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi, kampuni, shirika au taasisi inayofanya kazi kwa ajili ya kumuwakilisha muajiri wake;

"Waziri" maana yake ni Waziri anaehusika na Tawala za Mikoa na Serikali za mitaa.

"Zizi" maana yake ni sehemu ya kuhifadhia wanyama kama itakavyotengwa na Mamlaka ya Serikali ya Mtaa.

## SEHEMU YA PILI
## UHIFADHI WA MAZINGIRA NA UKUSANYAJI WA TAKA

Usafi wa mazingira.

3. Mtu yeyote anaeishi au kutumia eneo la Mamlaka ya Serikali ya Mtaa ana wajibu wa kuhifadhi na kuweka safi mazingira yake

Marufuku kutupa taka.

4.-(1)Hakuna mtu atakaetupa, kuweka, kusababisha au kuruhusu kutupwa katika maeneo ya makaazi uchafu wowote, kinyesi, takataka, mawe, au aina yoyote ya taka.

(2) Itakuwa ni wajibu wa kila mkaazi wa eneo ambae kwa makusudi au kwa uzembe anatupa taka au anasababisha kutupwa taka,kusafisha, kuondosha ,na kuweka katika hali nzuri ambayo mamlaka itaridhika.

Wajibu wa ukusanyaji na utupaji taka.

5.-(1) Kila Serikali ya Mtaa au Wakala wake itakuwa na jukumu la kukusanya, kusafisha na kuzoa taka zote zilizomo ndani ya eneo la Mamlaka ya Serikali ya Mtaa.

(2) Mtu yeyote anaezalisha taka katika nyumba, duka, kiwanda, gereji na sehemu nyengine yoyote ndani ya eneo la Serikali ya Mtaa anatakiwa azipeleke taka hizo katika maeneo yaliyotengwa au chombo kilichowekwa kwa kuhifadhia taka hizo.

Isipokuwa kwamba pale ambapo hakuna maeneo yaliyotengwa kwa ajili hiyo mtu huyo anatakiwa achimbe shimo kwa kuzihifadhi taka au azihifadhi kama atakavyoelekezwa na Mamlaka ya Serikali ya Mtaa.

(3) Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya kanuni hii atakuwa ametenda kosa na ikithibitika atalazimika kulipa faini isiyopungua Tsh 50,000 kwa kosa la kwanza na Tsh. 100,000 kwa kosa la pili au zaidi ya Tsh. 100,000 au kutumikia kifungo kisichopungua wiki mbili au adhabu zote mbili.

Ada ya usafi.

6. Mtu yeyote aneishi au anaefanya shughuli zake za kiuchumi na kijamii ndani ya eneo la Mamlaka ya Serikali ya Mtaa atawajibika kulipa ada ya usafi katika Serikali ya Mtaa kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Kanuni hizi.

Majivu ya moto, taka za maji maji n.k

7. Ni marufuku kwa mtu yeyote kuweka au kusababisha kuweka katika chombo au sehemu ya kuhifadhia taka majivu ya moto, taka za maji maji au kitu chengine chochote ambacho kinaweza kusababisha moto au athari kwa jamii au kwa chombo cha Serikali ya Mtaa.

Scanned with CamScanner

Utupaji taka baharini.

8. Ni marufuku kwa mtu yeyote kutupa taka ufukweni au baharini.

Utupaji taka na maji taka katika mitaro.

9.-(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kutupa taka ngumu na maji taka (machafu) katika mitaro ya serikali.

(2) Mtu yeyote anaishi karibu na mitaro ya serikali ndani ya mita hamsini (50) atahitajika kuunganisha mtaro wake katika mtaro wa serikali na kulipa ada kama ilivyoonyeshwa katika jadueli la namba 2 la kanuni hii.

Uchimbaji wa karo na vyoo.

10. Mtu yoyote, Kampuni au Shirika atakaekuwa anaishi ndani ya eneo la Mamlaka ya Serikali ya Mtaa atawajibika kuchimba karo kwa kuhifadhia maji taka kuweka choo ndani ya nyumba yake.

Serikali ya Mtaa inaweza kuweka vyombo vya kutilia taka.

11. Serikali ya Mtaa kwa malipo yalioekwa, inaweza kutoa kwa mkaazi ,wa eneo au mtu mwengine yeyote,taasisi au kampuni ,vyombo vya kukusanyia taka za biashara au za viwandani na kumpa taarifa ya notisi inaweza kumtaka mmiliki huyo kuweka taka kwenye chombo cha kuhifadhia taka ambavyo vitakuwa katika aina na idadi kama inavyoweza kufafanuliwa katika notisi au itakavyoelezwa venginevyo.

Wajibu wa kufunika vyombo vya kuwekea taka.

12.-(1)Kila mkaazi wa eneo la Mamlaka ya Serikali ya Mtaa atalazimika kufunika vyombo vya kuhifadhia taka wakati wote katika eneo la Mamlaka ya Serikali ya Mtaa.

(2) Ni wajibu wa gari lolote inayobeba au inayosafirisha taka kuzifunika taka hizo.

Kuchakura na kutawanya taka zilizokusanywa.

13. Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchakura au kutawanya taka zilizokusanywa katika vyombo vya kuhifadhia taka isipokuwa mfanyakazi aliyeajiriwa kwa kutekeleza kazi hizo.

Uharibifu wa vyombo vya kuhifadhia taka.

14.-(1) Mtu yeyote kwa makusudi atakaeondoa, atakaeharibu au kusababisha hasara kwa chombo chochote cha kuwekea taka kilichowekwa au kujengwa na Mamlaka husika katika mtaa au sehemu yoyote kwa ajili ya kuhifadhia au kukusanyia taka atakuwa ametenda kosa na ikithibitika atalazimika kulipa gharama za kurejesha haiba ya chombo hicho au kufanya matengenezo au kutumikia kifungo kwa muda wa miezi sita au adhabu zote mbili kwa pamoja.

(2) Kila mfanya biashara katika eneo la Mamlaka atalazimika kuweka chombo cha kuhifadhia taka katika eneo lake la biashara.

Uhifadhi wa Masalia ya vyombo vya moto, umeme, magari ya ng`ombe na marikwama.

15.-(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuweka au kusababisha kuweka katika maeneo ya wazi, masalia ya vyombo vya moto, umeme, magari ya ng`ombe na marikwama na vyuma chakavu.

(2) Mtu yeyote, kampuni au shirika litakalokiuka kifungu cha kanuni ndogo ya (1) atakuwa ametenda kosa akipatikana na hatia atalipa faini ya Tsh laki mbili na elfu hamsini, au kutumikia kifungo kwa muda wa mwezi mmoja au adhabu zote mbili kwa pamoja

Scanned with CamScanner

Kutupa taka, majitaka sehemu isioruhusika.

**16.** Ni marufuku kwa mtu yeyote kutupa kitu chochote kilichooza, kuharibika au kuruhusu uchafu wowote, maji machafu kutiririka katika mtaa, njia ya waendao kwa miguu, sehemu za wazi au pahala pa mjumuiko wa watu au sehemu isioruhusiwa na Sheria au Mamlaka ya Serikali za Mitaa au Taasisi nyengine ya Serikali.

Mmiliki kusafisha eneo linalomzunguka.

**17.**-(1) Mtu yeyote anaemiliki nyumba, kiwanja cha kujengea nyumba, boma, au msingi wa aina yoyote katika eneo la Mamlaka ya Serikali ya mtaa atalazimika kusafisha eneo hilo muda baada ya muda.

(2) Iwapo mmiliki atashindwa kusafisha eneo lake kwa muda wa wiki moja baada ya kupewa notisi, Serikali ya Mtaa itasafisha eneo hilo na kumtaka mmiliki kulipa gharama zote za usafishaji na faini isiozidi laki mbili,au kutumikia kifungo kisichopungua wiki tatu.

Utupaji taka kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuombwa.

**18.** Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa maombi ya mmiliki au mkaazi wa eneo lolote anaweza kuzoa taka kwa malipona kuzipeleka pale ambapo mkaazi wa eneo au mmiliki wa eneo ana wajibu, mahitaji ya kuzipeleka,na Serikali ya Mtaa itastahiki kulipwa gharama za uzoaji na utupaji wa taka hizo kwa kiwango kama itakavyoweka na Serikali ya Mtaa muda baada ya muda

Kuondoa taka kwa kuombwa.

**19.** Serikali ya Mtaa kama itaombwa na mkaazi wa eneo au mmiliki wa eneo inaweza kwa malipo yatakayoidhinishwa na Baraza kuondosha taka zitokanazo na kazi za ujenzi, bustani, taka ngumu zozote kutoka katika viwanda vyovyote, karakana, au maeneo ya biashara kwa malipo yatakayolipwa na mkaazi wa eneo au mmiliki wa eneo hilo muda baada ya muda kama itakavyopangwa na Mkurugenzi wa Mamlaka.

Vitu visivofaa kutupwa mitaani.

**20.**-(1) Hakuna mtu atakaeweka au kusababisha kuweka, kutupa au kuacha uchafu, karatasi, chupa, kopo, masalia ya mabati, vifaa vya ujenzi, maji yenye masalia ya chakula, matawi ya miti, magari au marikwama yasiotumika au takataka za aina yoyote katika mtaa wowote, njia za miguu, sehemu za mjumuiko wa watu au sehemu za wazi.

(2) Serikali ya Mtaa inaweza kuondoa au kusababisha kuondolewa uchafu huo, karatasi, chupa, kopo, vibati, masalia ya mabati, vifaa vya ujenzi, maji ya masalia, au takataka na kuzitupa itakapoona inafaa na kutoza fidia kwa mtu atakaekiuka kanuni hizi.

Taka za vigae

**21.**-(1) Hakuna mtu atakae tupa, kuweka, au kuacha chupa, vigae vibovu, au kitu chochote chenye ncha ndani au katika mtaa, njia ya wenda kwa mguu, sehemu ya mjumuiko wa watu sehemu za wazi ambayo itapelekea kusababisha madhara kwa wendao kwa miguu au wanyama au kusababish hasara kwa mali.

(2) Mtu yeyote atakaekwenda kinyume na Kanuni ndogo ya kwanza (1) atakuwa ametenda kosa na atalazimika kulipa faini isiyopungua 100,000/-.

Taka za vitu chakavu.

**22.** Mtu yeyote hatoruhusiwa kuweka taka zozote zinazotokana na vitu chakavu katika maeneo ya wazi, barabara, pembezoni mwa barabara na

Scanned with CamScanner

katika mitaa isipokuwa kwa ruhusa maalumu kutoka kwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali ya Mtaa husika.

Adhabu.

23. Mtu yeyote atakae kwenda kinyume na kanuni ya 22 ya kanuni hii atakuwa ni mkosa na ikithibitika atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi za kitanzania laki tano au kifungo kisichopungua miezi mitatu au vyote viwili kwa pamoja.

Uchimbaji wa mchanga.

24.-(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchimba mchanga katika eneo lisiloruhusiwa.

(2) Mtu yeyote atakaekamatwa anaharibu mazingira kwa kuchimba mchanga katika sehemu zisizoruhusiwa atakuwa ametenda kosa na ikithibitika atalazimika kulipa faini ya shilingi laki tano Tsh. 500,000/-.

(3) Mtu yoyote atakaekamatwa kwa kosa la kuchimba mchanga chombo chochote alichokitumia kubebea mchanga atalazimika kukikomboa chombo hicho kwa kulipa faini isiyopungua Tsh. 300,000 au vyombo hivyo vitataifishwa na Mamlaka ya Serikali ya Mtaa.

Marufuku kuchimba mtaani.

25.-(1) Hakuna mtu atakaeharibu sura ya ardhi katika mtaa, njia au kuchimba, kusababisha kuchimbwa shimo, handaki, au tundu kwa madhumuni yoyote au vyenginevyo katika au mtaa, njia au sehemu zinazo tembelewa na watu au sehemu ya wazi bila ya ruhusa ya maandishi kutoka kwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali ya Mtaa kwa kuzingatia mipaka na masharti ya kibali au ruhusa hio.

(2) Mtu yeyote ambae amepata ruhusa ya Mamlaka ya Serikali ya Mtaa kufanya kazi ambazo zimetajwa katika kifungu cha (1) kama kuacha shimo lolote, chimbo, handaki au mambo mengine ya hatari karibu au katika mtaa, njia, sehemu zinazotembelewa na watu au sehehmu za wazi bila ya kuweka uzio au kuwasha taa inawaka ndani ya eneo hilo kuanzia kuzama kwa Jua hadi kuchomoza.

(3) Bila kuathiri sheria nyingine zinazo tumika Zanzibar kanuni hizi hazitotumika kwa mtu yoyote au chombo chenye Mamlaka kisheria ambacho kimeruhusiwa kutekeleza kazi hizo kwa madhumuni ya matengenezo, ukarabati, upanuzi, na ubadilishaji wa mabomba, michirizi, makaro au misingi inayotumika kwa usambazaji au uhifadhi wa huduma za jamii.

Uchimbaji, uchongaji wa matofali ya mawe, fusi na kokoto.

26. Hakuna mtu, kampuni au shirika litakalofanyakazi ya uchimbaji mawe, fusi, kokoto. Udongo na vitu vinavyoshabihiana navyo bila ya kupata kibali kutoka Mamlaka ya Serikali ya Mtaa.

Udhibiti wa vyombo vya moto na magari katika maeneo ya mji.

27.-(1) Mtu yoyote hatoruhusiwa kuweka chombo chochote cha moto katika maeneo ya wazi, maegesho ya magari, barabarani au pembezoni mwa barabara kwa zaidi ya masaa kumi na mbili bila ya kupata ruhusa maalumu kutoka kwa Mkurugenzi wa Mamlaka husika.

(2) Mamlaka za serikali za Mitaa zitaondosha chombo au gari lolote ambalo litakaloekwa kinyume na kanuni hizi na mmiliki atawajibia kulipa gharama za uondoshwaji wa chombo au gari hilo.

Scanned with CamScanner

(2) Mtu yoyote atakaekwenda kinyume na kanuni ya 27 ya kanuni hii atakuwa ametenda kosa na ikithibitika kulipa faini isiyopungua laki moja au kifungo kisichozidi miezi mitatu au adhabu zote kwa pamoja.

Marufuku kwa vyombo na wanyama kupita kwenye njia za wenda kwa miguu.

28. Hakuna mtu atakaepanda au kuendesha au kusukuma chombo au kuendesha farasi, ngombe, ngamia, punda au kuruhusu mnyama huyo au chombo hicho kubakia katika njia yoyote ya wendao kwa miguu katika eneo la Mamlaka za Serikali za Mitaa za Mijini.

Sehemu za hatari kuwekwa salama.

29. Mamlaka za Serikali za Mtaa inaweza kumtaka mtu mwenye ardhi yoyote au sehemu ambayo ina shimo, kisima, handaki, au sehemu ya hatari ya wapita njia kulifukia, kulifunika au kuliwekea uzio.

Adhabu.

30. Mtu yeyote atakaekwenda kinyume na vifungu vya sehemu hii ambapo adhabu yake haijaainishwa, atakuwa ametenda kosa na ikithibitika atalazimika kulipa faini isiyopungua shilingi laki tano 500,000 Tsh/- na isiyozidi laki nane 800,000 Tsh/- au kutumikia adhabu ya kifungo kisichopungua miezi mitatu na kisichozidi miezi sita au adhabu zote mbili kwa pamoja.

## SEHEMU YA TATU
## UTARATIBU WA UTOWAJI WA LESENI ZA BIASHARA

Ukataji wa leseni.

31.-(1) Bila ya kuathiri Sheria ya leseni za Biashara Namba 13 ya 2014 na Sheria nyenginezo, mtu yeyote anaefanya biashara ya huduma au bidhaa ndani ya eneo la Serikali ya Mtaa anatakiwa akate leseni katika Serikali ya Mtaa husika.

(2) Mtu yeyote anayekusudia kufanya biashara atalazimika kulipia na kujaza fomu ya maombi ya leseni kama inavyoeleza kwenye Jadweli la Kanuni hizi na kuambatanisha na uthibitisho wa kulipa kodi kwa mujibu wa sheria za Fedha na Kodi.

(3) Iwapo mfanyabiashara analazimika kupata kibali au ruhusa maalum kutoka Mamlaka husika itamlazimu ajaze fomu ya maombi na aiambatane na kibali au ruhusa hiyo.

Malipo ya leseni

32. Kila Mfanyabiashara anaefanya biashara katika eneo la Serikali ya Mtaa atalazimika kulipia malipo ya leseni kama yalivyooneshwa katika Jadweli la Kanuni hizi.

Biashara za kwenye magari, mikokoteni na vyombo vya maringi mawili.

33. Mtu yoyote, Kampuni au Shirika litakalokuwa linafanya biashara kwa kutumia vyombo vya usafiri vya moto, baiskeli, mkoteni atalazimika kukata leseni kutoka Mamlaka ya Serikali ya Mtaa ambayo biashara itakapokuwa inafanyika.

Ada ya biashara ndogo ndogo.

34. Mtu yeyote anaefanya biashara ndogo ndogo katika maeneo yaliyotengwa na Serikali ya Mtaa kwa madhumuni hayo atalazimika kuchangia ada ya huduma maalum kama inavyoonekana katika Jadweli la Kanuni hizi.

Scanned with CamScanner

(2) Kila mfanya bishara katika eneo la Mamlaka za Serikali za Mitaa alazimika kuhifadhi bidhaa zake anazoziuza kwa unadhifu na kuzingatia masharti ya usalama wa afya kwa watumiaji .

(3)Mtu yeyote atakaenda kinyume na kanuni hii atakuwa ametenda kosa na ikithibitika atalazimika kulipa faini isiopungua shilingi laki tatu(300,000/) au kutumikia kifungo kisichopungua miezi mitatu.

35. Mamlaka ya Serikali ya Mtaa iliyo toa leseni inaweza kusitisha matumizi ya leseni likitokea jambo au mambo yafuatayo:- *Kusitishwa kwa leseni ya biashara.*

(a) iwapo kibali au ruhusa iliyotolewa na Mamlaka husika imemaliza muda wake;

(b) iwapo Mfanyabiashara ameomba kusitisha leseni yake; na

(c) iwapo atashindwa kutekeleza maelekezo aliyopewa na Mamlaka husika.

(d) iwapo mfanya biashara atabadilisha matumizi ya leseni alioruhusiwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa;

(e) iwapo atakiuka utekelezaji wa Sheria hii au nyenginezo zilizopo nchini;

36. Serikali ya Mtaa inaweza kufuta matumizi ya leseni katika mazingira yafuatayo:- *kufuta leseni ya biashara.*

(a) iwapo mfanyabiashara amekwenda kinyume na masharti yaliyowekwa katika kufanya biashara hiyo;

(b) iwapo mfanyabiashara ameitoa leseni yake na kumpa mtu mwengine kuitumia;

(c) iwapo mfanyabiashara atadanganya au atatoa taarifa za uongo kwa Mamlaka husika katika utaratibu wa ukataji na upatikanaji leseni yake; na

(d) iwapo mfanyabiashara atafanya uharibifu katika hati ya leseni ya biashara.

37. Mtu yeyote atakaepoteza leseni yake kwa njia moja au nyengineyo atatakiwa kufanya yafuatayo:- *Kupotea kwa leseni.*

(a) Kutoa taarifa kituo chochote cha Polisi;

(b) Kutoa taarifa katika Ofisi ya Mamlaka na kueleza sababu za kupotea kwa Leseni hiyo;

(c) atalazimika kujaza fomu ya kuombea leseni; na

(d) kulipa malipo ya asilimia hamsini 50% ambayo ni thamani ya leseni yake ya mwanzo.

Scanned with CamScanner

Utaratibu wa Ukaguzi wa maeneo ya biashara.

38.-(1) Ni jukumu la Mamlaka kufanya ukaguzi katika maeneo yote ya Mamlaka ya Serikali ya Mtaa yanayotakiwa kupatiwa leseni za biashara.

(2) Afisa ukaguzi wa Mamlaka atakagua maeneo yote yanayofanywa biashara katika wakati unaofaa.

(3) Afisa ukaguzi atatakiwa kujaza fomu maalum juu ya kile alichokikagua na alichokigundua kutokana na ukaguzi alioufanya.

(4) Afisa ukaguzi anaweza kufanya ukaguzi muda wowote ndani ya maeneo ya biashara ya Mamlaka husika kwa siku za kazi na siku za mapumziko.

(5) Mfanya biashara atalazimika kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Afisa na kulipa shilingi elfu tano (Tsh. 5,000/-) ikiwa ni ada ya ukaguzi na kupatiwa risiti ya malipo aliyoyafanya.

(6) Mfanyabiashara yeyote atakaekataa kutoa ushirikiano, au kutumia lugha chafu kwa Afisa, kutoiweka leseni katika sehemu ya biashara au kumfukuza Afisa atakuwa ametenda kosa na ikithibitika atalipa faini ya shilingi laki moja (Tsh. 100,000/-) au kutumikia kifungo kwa muda wa miezi miwili au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Afisa kubadili kiwango cha leseni.

39.-(1) Ni marufuku kwa Afisa au Afisa aliyeidhinishwa na Mamlaka kubadili kiwango cha leseni isipokuwa kwa maelekezo atakayopewa na Mkurugenzi wa Mamlaka au Kamati ya Fedha inayoidhinisha viwango hivyo na kupitishwa na Baraza.

(2) Afisa yeyote atakaekwenda kinyume na kifungu hiki atakuwa ametenda kosa la kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake ikithibitika Afisa huyo atalazimika kulipa punguzo la leseni hiyo au kurejesha nyongeza kwa mkataji leseni.

Adhabu.

40.-(1) Mtu yeyote atakaefanya biashara zake bila ya kuwa na leseni halali atakuwa ametenda kosa na ikithibitika atalazimika kukata leseni, kulipa faini isiyozidi shilingi za kitanzania laki tano(Tsh.500,000/-) na faini isiyopungua shilingi za kitanzania laki mbili (Tsh. 200,000/-) au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu (3) au adhabu zote mbili kwa pamoja.

(2) Mtu yeyote atakayedanganya au katoa taarifa za uongo katika kupata leseni atakuwa ametenda kosa na akithibitika atalazimika kulipa faini isiyopungua shilingi za kitanzania 400,000 na isiyozidi shilingi za kitanzania laki tano (Tsh. 500,000/-).

(3) Mtu yeyote atakaefanya biashara kwa kutumia leseni ya mtu mwengine atakuwa ametenda kosa na akithibitika atalazimika kulipa faini isiyozidi shilingi za kitanzania laki tano na hamsini elfu (Tsh. 550,000/-) na isiyopungua shilingi za kitanzania laki nne na hamsini elfu (Tsh. 450,000/-).

(4) Mtu yeyote atakayeshindwa kumpa mkaguzi wa Mamlaka leseni yake ya biashara wakati wa ukaguzi atakuwa ametenda kosa na akithibitika atalazimika kulipa faini isiyopungua shilingi za ki...

Scanned with CamScanner

Hamsini (Tsh. 150,000/-) na isiyozidi shilingi za kitanzania laki mbili (Tsh. 200,000/-).

41. Hakuna mtu atakaefanya mnada, kuuza au pendekezo la kuuza, kufanya biashara yoyote katika mtaa, njiani, pahala pa mjumuiko wa watu, maeneo ya wazi bila ya kibali cha maandishi kutoka kwa Mkurugenzi wa Serikali ya Mtaa, na kwa masharti yalioelezwa ndani ya kibali hicho. Maarufuku kufanya biashara Mtaani.

42. Hakuna mtu yeyote atakae ruhusiwa kuuza kitu chochote sehemu ya njia ya wenda kwa miguu, mtaa, sehemu za mjumuiko wa watu au sehemu za wazi kwa muda mrefu zaidi ya muda wa lazima au muda wa lazima kwa kupakia na kupakua, na kwa vyovyote vile hakutakuwa na sababu yoyote itakayo kubalika baada ya kupewa notisi ya kuondosha kutoka eneo hilo na askari polisi au afisa wa Mamlaka za Serikali ya Mtaa. Bidhaa kuacha kwa muda mrefu katika mitaa.

43. Hakuna mtu atakaeonesha biashara kwa ajili ya kutangaza bidhaa hio au kuzitundika kwenye njia, mtaa au sehemu ya mjumuiko wa watu mpaka apate kibali cha maandishi kutoka kwa Mkurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kuninginiza Bidhaa Mitaani.

44.-(1) Mtu yeyote atakaemiliki au kufuga mnyama katika maeneo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa katika eneo la Manispaa atalazimika kukata leseni kwa mwaka kwa ajili ya umiliki wa mfugo huo na kupatiwa risiti maalum. Leseni za wanyama.

(2) Mtu yeyote ataekwenda kinyume na kanuni ya 44(1) ya kanuni hii atakuwa ametenda kosa na ikithibitika atalazimika kulipa faini ya shilingi za kitanzania laki tatu (Tsh. 300,000/-).

45.-(1) Mtu yeyote anayefanya biashara ya kubeba mizigo kwa kutumia gari linalokokotwa na mnyama, Binadamu au kusambazwa na gari ya mkokoteni ndani ya Mamlaka atalazimika kukata leseni kila mwaka kwa shilingi za kitanzania elfu ishirini na tano (Tsh. 25,000/-). Leseni ya gari linalokokotwa na mnyama, Binadamu au kusambazwa na gari.

(2) Mtu yeyote atakaekiuka masharti ya kifungu (1) cha kanuni hii atakuwa ametenda kosa na ikithibitika atalazimika kulipa faini ya shilingi za kitanzania elfu hamsini (Tsh. 50,000/-) na akishindwa atatumikia kifungo cha mwezi mmoja.

46.-(1) Ni marufuku kuweka, kuchora, kuandika au kubandika tangazo la biashara katika maeneo ya wazi, pembezoni mwa barabara, katika majengo, kwenye gari, katika kuta au sehemu nyengine bila ya kibali kutoka katika Mamlaka ya Serikali ya Mtaa. Tangazo la biashara.

(2) Kibali hicho kitatolewa kwa malipo ya siku au mwaka kulingana na ukubwa, ubora au muonekano watangazo kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Kanuni hizi.

(3) Mfanya biashara atakaekua na zaidi ya tangazo moja atalazimika kulipia kwa kila tangazo.

Scanned with CamScanner

(4) Mfanyabiashara yeyote atakaekwenda kinyume na kanuni ya 46 (1), (2) au (3) ya kanuni hii atakuwa ametenda kosa na ikithibitika atalipa ada ya tangazo na faini ya asilimia hamsini (50%) ya malipo ya kibali au gharama aliyotakiwa kukilipia.

Matangazo ya Kampuni.

47. Kampuni au Shirika lolote litakalo weka tangazo katika eneo la Mamlaka ya Serikali ya Mtaa litalazimika kukata kibali cha kuweka tangazo na litalazimika kulipia tangazo hilo kila mwaka kama inavyoelezwa katika Jaduweli la Kanuni hizi.

Ada ya mnada.

48.-(1) Mtu yeyote anayenadisha bidhaa katika eneo la Mamlaka atalazimika kulipia kila mwaka ada ya udalali wa minada ya shilingi za kitanzania laki moja (Tsh. 100,000) ikiwa ni malipo ya beji a kibali kwa mwaka.

(2) Mtu yeyote anayenadishiwa bidhaa yake katika eneo la Mamlaka anatakiwa alipe ada ya mnada asilimia tano (5%) ya kila bidhaa anayonadishwa.

(3) Mtu yeyote ambae amefanya malipo chini ya kanuni hii atalazimika kupatiwa risiti inayoonesha kiwango cha fedha za malipo aliyofanya.

## SEHEMU YA NNE
## HUDUMA ZA USAFIRI

Vituo vya Daladala.

49.-(1) Itakuwa jukumu la Mamlaka au Wakala kujenga, kuimarisha na kuvisimamia vituo vya Daladala katika eneo la Serikali ya Mtaa.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuharibu, kuchora, kuvunja vituo vya Daladala.

(3) Mtu yeyote ataekwenda kinyume na kanuni hii atakuwa ametenda kosa na ikithibitika atalazimika kurekebisha sehemu au eneo aliloharibu pamoja na kulipa faini isiyozidi shilingi laki saba (Tsh. 700,000/-) na akishindwa kurekebisha na kulipa faini atatumikia kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu.

Utambulisho wa ruhusa ya njia.

50.-(1) Mmiliki wa gari ya abiria atalazimika kupata ruhusa ya njia ya gari yake katika Afisi ya Mamlaka ya Serikali ya Mtaa ambako gari hilo linafanyia kazi na atapatiwa stika ambayo atalazimika kuibandika katika sehemu ya wazi ya gari yake.

(2) Mtu yeyote anaemiliki gari ya abiria na akaifanyia kazi katika eneo la Mamlaka atalazimika kulipia ada ya ruhusa ya njia isiopungua Shilingi elfu hamsini (Tsh. 50,000/-) kwa mwaka na kama itakavyopangwa na Baraza muda baada ya muda.

(3) Mtu yeyote atakaegundulika kufanya kazi ndani ya maeneo ya Mamlaka bila kulipia ada ya ruhusa ya njia atakuwa ametenda kosa na ikithibitika atalipa faini ya Shilingi laki mbili (Tsh. 200,000/-) au kutumikia kifungo kwa muda wa mwezi mmoja au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Scanned with CamScanner

(4) Mtu yeyote atakaemiliki gari ya biashara kibinafsi atalazimika kulipia ada ya njia isiyopungua 3000 kwa siku, katika Mamlaka husika.

(5) Mtu yeyote atakaekuwa anafanya kazi ya kusafirisha abiria ndani ya eneo la Serikali ya Mtaa atalazimika kulipa ada ya kiingilio katika Wilaya kama ilivyoanishwa katika Jadueli la kwanza la Kanuni hizi.

Utoaji na matumizi ya beji.

51.-(1) Dereva au Utingo wa gari ya abiria inayotoa huduma katika eneo ya Mamlaka wanalazimika kuvaa beji inayotolewa na Mamlaka ya Serikali ya Mtaa katika Wilaya husika wakati wa kutoa huduma.

(2) Kila Dereva au Utingo atawajibika kulipa 50,000/- kila mwaka kwa kupatiwa beji katika Afisi ya Mamlaka.

(3) Dereva au utingo yeyote ambae hatovaa beji wakati wa kazi atakuwa ametenda kosa na ikithibitika atatozwa faini ya Shilingi laki moja na elfu hamsini (Tsh.150,000/-) au atatumikia kifungo kwa muda usiozidi mwezi mmoja au adhabu zote mbili kwa pamoja

Uwekaji wa Alama za rangi kwa gari za abiria.

52. Mamlaka ya Serikali ya Mtaa itaweka utaratibu na kuweka alama za rangi kwa magari yote yanayotoa huduma ya usafiri katika maeneo ya Serikali ya Mitaa;

Mtu yoyote atakaekuwa anatoa huduma ya usafiri kwa abiria bila ya kuweka alama ya rangi ya gari la abiria kwa mujibu wa utaratibu wa Serikali ya Mtaa atakuwa ametenda kosa, akipatikana na hatia atalipa faini isiopungua Tsh. 300,000/- au kutumikia adhabu ya kifungo kisichopungua miezi miwili,na atalazimika kuweka rangi katika gari ya abiria inayotoa huduma ya usafiri katika eneo la Serikali ya Mtaa Husika.

Ada ya kuhaulisha Ardhi.

53.-(1) Bila ya kuathiri sheria ya uhaulishaji wa Ardhi namba 8 ya 1994, mtu yeyote anaehaulisha Ardhi katika eneo la Mamlaka atalazimika kulipa asilimia 1% ya thamani ya kitu husika kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

(2) Mtu yeyote atakaekwenda kinyume na kanuni hii atakuwa ametenda kosa na ikithibitika atalazimika kulipa faini isiyopungua Tsh.1000,000/= na kulazimika kutekeleza agizo hilo au atatumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua muda wa wiki tatu.

Ada ya Ujenzi.

54.-(1) Mtu yeyote anaetaka kujenga banda, nyumba au ujenzi wa aina yoyote katika eneo la Mamlaka, atalazimika kujaza fomu maalum iliyoambataninishwa katika Jadweli la Kanuni hizi na mchoro wa ujenzi huo na kulipia ada ya ujenzi kama ilivyoainishwa katika Kanuni hizi

(2) Mtu yeyote atakaekwenda kinyume na maelekezo ya ujenzi atakayopewa na Mamlaka atakuwa ametenda kosa na ikithibitika Mamlaka itamtaka avunje ujenzi huo na akishindwa Mamlaka itavunja na gharama za ubomoaji zitakuwa ju ya mmiliki wa jengo hilo.

Uwekaji wa miundo-mbinu.

55. Mtu yeyote, Kampuni au Shirika atakaekuwa anataka kutumia maeneo ya Mamlaka za Serikali ya Mtaa kwa ajili ya kusambaza miundombinu ya mawasiliano au huduma za kijamii ya aina yoyote kwa kuchimba au vyenginevyo atalazimika kutoa taarifa katika Mamlaka husika na kupata kibali cha ruhusa ya kazi hiyo

Scanned with CamScanner

Adhabu ya jumla.

**56.** Mtu yeyote atakaepatikana na hatia ya kutenda kosa ambalo adhabu yake haijatajwa katika sehemu hii ya kanuni atalipa faini ya shilingi za kitanzania zisizopungua Tsh. 2000,000/- na isiyozidi milioni tano Tsh. 5000,000/- au atatumikia kifungo kwa muda usiopungua miezi miwili (2) na usiozidi miezi sita (6).

## SEHEMU YA TANO
## UDHIBITI WA MAZAO YA MISITU NA MALIASILI

Ada ya mazao ya misitu.

**57.**-(1) Mvunaji wa mazao ya misitu atalazimika kulipa ada katika Mamlaka baada ya kuruhusiwa na kupata kibali kutoka katika Mamlaka.

(2) Ada ambayo inastahili kulipwa kwa mujibu wa kanuni ya kanuni hii itakuwa kama ambavyo imeainishwa katika Jadweli la Kanuni hizi

(3) Iwapo mvunaji wa mazao ya misitu atashindwa kufuata sharti la kanuni hii atalazimika kulipa faini ambayo ni mara mbili ya ada anayopaswa kulipa au kutumikia adhabu ya kifungo isiyopungua wiki moja.

Ada ya mazao ya Maliasili.

**58.**-(1) Mvunaji wa maliasili zisizorejesheka analazimika kulipa ada katika Mamlaka baada ya kuruhusiwa na kupata kibali kutoka Mamlaka husika.

(2) Ada ambayo inastahili kulipwa kwa mujibu wa kanuni (1) ya kanuni hii itakuwa kama ambavyo imeainishwa katika Jadweli la Kanuni hizi.

(3) Iwapo mvunaji wa maliasili zisizorejesheka atashindwa kufuata sharti la kanuni hii atalazimika kulipa faini ambayo ni mara mbili ya ada anayopaswa kulipa.

Ada ya kusafirisha mazao ya baharini.

**59.**-(1) Mtu yeyote anaesafirisha mwani ndani ya Mamlaka analazimika kulipa ada ya Tsh. 2000/- kwa tani moja la mwani.

(2) Mtu yeyote atakaekwenda kinyume na kanuni 52(1) ya kanuni hii atakuwa ametenda kosa na ikithibitika atalazimika kulipa faini ya Tsh. 300,000/- na akishindwa kulipa faini, Mamlaka italizuia gari lake kusafirisha mwani kwa kulikabidhisha kituo cha Polisi hadi atakapolipa.

Ada ya kukodisha mikarafuu.

**60.** Mtu yeyote anaemiliki mikarafuu, mishokishoki, minazi, midoriani, miembe, mifenesi na mimea inayolingana na kuikodisha atalazimika kulipia ada ya ukodishaji katika Mamlaka iliyopo mimea hiyo muda baada ya muda kama itakavyopangwa na Mamlamka.

## SEHEMU YA SITA
## ADA ZITOKANAZO NA KODI AU PANGO

Taarifa ya kukodisha mali zinazohamishika na zisizohami-

**61.**-(1) Mmiliki yeyote wa mali atatakiwa atoe taarifa ya kukodisha mali yake katika Mamlaka husika.

(2) Mmiliki wa mali inayopangishwa atalazimika kulipa asilimia

Scanned with CamScanner

inayohamishika au isiyohamishika katika eneo la Mamlaka ya Serikali ya Mtaa .

(3) Iwapo mmiliki wa mali iliyopangishwa atashindwa kulipa ada hiyo atakuwa ametenda kosa na ikithibitika atalazimika kulipa faini ya isiyopungua shilingi laki tano (Tsh.500, 000/-) na isiyozidi shilingi laki nane Tsh.800, 000/- au kutumikia kifungo kwa muda usiopungua miezi minne.

62.-(1)Mtu yeyote atakayekodisha sehemu ya ardhi kwa ajili ya ujenzi wa mnara anatakiwa atoe taarifa ya kukodisha sehemu hiyo katika Mamlaka husika. Mkodishaji wa ardhi kwa ujenzi wa mnara.

(2) Mamlaka itamtaka mkodishaji huyo kulipa asilimia tano (5%) ya pato ya kodi kwa mwaka ikiwa ni ada ya ukodishaji sehemu hiyo.

(3) Iwapo mkodishaji wa mnara atashindwa kulipa ada hiyo atakuwa ametenda kosa na ikithibitika atalazimika kulipa asilimia ya pato la kodi au faini isiyopungua shilingi (Tsh. 1000, 000/-) na isiyozidi shilingi milioni tatu (Tsh. 3000,000/- au kutumikia kifungo kwa muda usiopungua miezi sita.

63.-(1) Mtu yeyote anaejenga, kuweka au kuhamisha mnara sehemu moja kwenda nyengine katika eneo la Mamlaka anatakiwa kulipa milioni tatu (3000,000/-) ikiwa ni ada ya ujenzi wa mnara huo. Ada ya ujenzi mnara na uendeshaji.

(2) Mtu yeyote anaemiliki mnara wa mawasiliano katika eneo la Mamlaka atalazimika kulipia uendeshaji wa mnaara shilingi 2,500,000 kwa kila mwaka

(3) Iwapo mjenzi wa mnara huyo atashindwa kulipa ada hiyo atakuwa ametenda kosa na ikithibitika atalazimika kulipa faini isiyopungua shilingimilioni mbili (Tsh. 2000,000/-) na isiyozidi shilingi milioni tano (Tsh. 5,000,000/-) au kutumikia kifungo kwa muda usiopungua miezi sita

64.-(1) Mtu yeyote atakaewekeza kitega uchumi katika eneo la Mamlaka atalazimika kulipa asilimia tano (5%) kutoka katika gharama za uwekezaji. Ada za Uwekezaji kitega Uchumi.

(2) Mtu yeyote atakaeshindwa kufanya malipo hayo atakuwa ametenda kosa na ikithibitika atalazimika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tatu. (Tsh. 3000,000/-) au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi miwili.

65.-(1) Mtu yeyote anaefanya shughuli za kibiashara katika eneo la diko atalazimika kulipa ada ya huduma katika diko hilo kama ilivyooneshwa katika Jadweli la Kanuni hizi. Ada ya diko.

(2) Mtu yoyote atakahamia Dikoni kwa shughuli za dago atalazimika kuwasilisha kibali cha ruhusa ya kuhamia kutoka sehemu aliotoka na kuwasilisha katika ofisi za Mamlaka za serikali za Mitaa.

Scanned with CamScanner

Usajili wa vyombo vya usafiri.

**66.** Mtu yoyote Kampuni au Shirika litakalokuwa linafanya kazi katika eneo la Mamlaka za Serikali za Mitaa shughuli za uvuvi, usafiri shaji wa mizigo, usafirishaji wa abiria kwa njia ya majini atalazimika kufanya usajili na kukata leseni kila mwaka katikaAfisi za Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuruhusiwa kutekeleza shughuli hizo ndani ya eneo la Mamlaka za Serikali za mitaa na atalazimika kulipa asilimia 2% ya mapato kutokana na mauzo tiketi kwa kila trip.

Mamlaka ya serikali ya Mtaa kuweka uwekaji wa Kumbu-kumbu.

**67.** Mamlaka ya Serikali ya Mtaa italazimika kuweka kumbukumbu za usajili wa vyombo vya usafiri wa majini vinavyotoa huduma ya usafiri vilivyomo katika eneo la Mamlaka ya Serikali ya Mtaa

## SEHEMU YA SABA
## UDHIBITI WA UZURURAJI WA WANYAMA

Ruhusa ya kufuga wanyama.

**68.** Hakuna mtu ataye tumia jengo lolote kwa ajili ya kufugia wanyama ndani ya eneo la Mji mpaka atakapo kuwa na kibali cha kuhifadhi wanyama hao kutoka mamlaka ya Serikali ya Mtaa husika.

(1) Mamlaka ya Serikali ya Mtaa inaweza kutoa kibali cha kufuga au kuhifadhi wanyama ndani ya mji kwa mtu yeyote ikiwa eneo lake imekidhi vigezo vya kuhifadhi wanyama husika.

(2) Hakuna mtu yeyote atakae funga mnyama wa porini katika eneo la Mamlaka isipokuwa kwa kibali maalumu kutoka kwa taasisi zinazo husika kabla ya kupewa kibali na Mamlaka ya Serikali ya Mtaa.

(3) Hakuna kibali cha kuhifadhi wanyama kitakacho tolewa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa za Mjini mpaka pale atakapo kuwa amekidhi vigezo vya kuhifadhi wanyama hao kwa mjibu wa sheria zinazo husiana na wanyama.

(4) Bila ya kuathiri Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali ya Wanyama Namba 11 ya mwaka 1999, Ni marufuku kwa mtu yeyote anaemiliki mnyama kumuachia anazurura ovyo ndani ya maeneo ya mji.

Uwezo wa kukamata mnyama.

**69.** Mamlaka ya Serikali ya Mtaa itakuwa na uwezo wa kukamata mnyama au wanyama wanaozurura ovyo ndani ya eneo lake.

Kuwapitisha na kufunga wanyama sehemu zisizoru-husika.

**70.** Mtu yeyote mwenye kumiliki mnyama na kumpitisha au kumfunga au kumuachia kuzurura ovyo sehemu zisizoruhusika atakuwa ametenda kosa na ikithibitika atalazimika kulipa faini yashilingi (350,000/-) au kifungo cha mwezi miezi mitatu. Sehemu zenyewe ni kama zifuatazo:-

(i) Hospitali,

(ii) Nyumba za ibada,

(iii) Viwanja vya michezo,

(iv) Skuli,

Scanned with CamScanner

(v) Nyumba za wageni,

(vi) Barabara kuu,

(vii) Maeneo ya wazi na maeneo yenye mjumuiiko wa watu,

(viii) Maeneo ya Mji, au

(ix) Sehemu za viazio vya maji safi.

71. Mmiliki yeyote wa gari la kukokotwa na mnyama atakaegundulika kumfanyisha kazi mtoto chini ya umri wa miaka 18 atakuwa ametenda kosa na ikithibiti atalipa faini isiyopungua shilingi laki tatu (Ths 300,000/-) au kutumikia kifungo miezi mitatu au adhabu zote mbili kwa pamoja. Kumfanyisha kazi mtoto chini ya umri wa miaka 18.

72.-(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote ambae anamiliki mnyama kwa kumfanyisha kazi bila ya kumpatia chakula, kumwendesha kwa mwendo wa haraka sana, kumbebesha mzigo mzito, kumuuza akiwa katika hali dhofu, kumtesa, kumpiga bakora au kumfanyia jambo lolote lile linaloondoa au kupunguza hadhi ya mnyama huyo. Kumtesa mnyama.

(2) Ni marufuku kumfanyisha kazi mnyama kuanzia saa kumi na mbili na nusu jioni (12:30 jioni) hadi saa kumi na mbili na nusu asubuhi (12:30 asubuhi)

(3) Mtu yeyote atakaekwenda kinyume na kanuni hii atakuwa ametenda kosa na ikithibitika atalazimika kulipa faini isiyopungua shilingi hamsini elfu (Tsh. 50,000/-) na isiyozidi shilingi laki mbili (Tsh. 200,000/-) au kutumikia kifungo kwa mwezi mmoja au adhabu zote mbili kwa pamoja..

73.-(1) Mnyama yoyote anaekamatwa anazurura ndani ya maeneo ya Mamlaka atapelekwa katika zizi maalum lililotengwa kwa ajili hiyo. Utaratibu wa mnyama aliekamatwa.

(2) Iwapo mmiliki wa mnyama atatokea kabla ya mnyama huyo hajafikishwa katika zizi, atalazimika kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja na hamsini elfu (Tsh. 150,000).

(3) Iwapo mnyama amesababisha hasara au uharibifu, mmiliki atalazimika kulipa gharama na fidia kwa mujibu wa hasara na uharibifu uliofanyika kwa mujibu wa tathmini ya gharama iliofanywa na mamlaka.

(4) Iwapo mnyama atakaekamatwa atafikishwa katika zizi, mmiliki atalazimika kulipa gharama za usafirishaji, ulishaji, matibabu na uhifadhi pamoja na faini isiyopungua shilingi laki tano (Tsh. 500,000).

(5) Iwapo mnyama huyo anahifadhiwa ndani ya zizi kwa muda wa wiki moja bila mmiliki kutokea, Mamlaka italazimika kumuuza mnyama huyo kwa njia ya mnada.

(6) Mnyama anaeuzwa na Mamlaka kwa njia ya mnada, fedha itakayopatikana itagawanywa kwa kufuata utaratibu ufuatao:-

Scanned with CamScanner

(a) kulipia gharama zote zilizotumika kwa mujibu wa uharibifu au hasara uliosababishwa na mnyama huyo,

(b) Kulipia gharama za mnada asilimia 5%,

(c) Kulipia gharama ya zizi, chanjo,

(d) Fedha zitakazobakia atarudishiwa mmiliki wa mnyama,

(e) Iwapo baada ya mnada, fedha zilizopatikana hazikuweza kufidia gharama zilizotumika, atakapotokea mmiliki atalazimika kuongeza gharama za ziada zilizotumika.

(f) Endapo mnyama atakamwatwa kwa mara ya pili na kuwekwa katika zizi lililotengwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa na mnyama huyo atafilisiwa na Mamlaka husika.

Kuwapatia wanyama chanjo.

74.-(1) Mtu yeyote anaemiliki au mwenye dhamana ya mnyama atawajibika kuwafikisha wanyama katika eneo lililoandaliwa na Mamlaka kwa kupatiwa kinga kulingana na tangazo na utaratibu utakaopangwa na Mamlaka husika na kutolewa muda baada ya muda.

(2) Mmiliki au mwenye dhamana ya mnyama atalazimika kulipa gharama zote zinazohitajika katika kupatiwa huduma hiyo.

Maeneo ya majosho.

75.-(1) Kila Mamlaka itatenga maeneo maalum kwa ajili ya majosho ya wanyama.

(2) Mmiliki au mwenye dhamana ya mnyama atalazimika kumpeleka mnyama wake katika eneo la josho lililowekwa na Mamlaka kwa ajili ya kumkinga maradhi.

(3) Mtu yeyote atakakwenda kinyume na Kanuni ya 74(1)(2) na 75 (1)(2) atakuwa ametenda kosa akipatikana na hatia atalazimika kulipa faini isiyopungua shilingi 300,00 za kitanznia au kutumikia kifungu cha miezi mitatu.

## SEHEMU YA NANE
## MAEGESHO YA VYOMBO VYA MOTO

Kuegesha na kupakia.

76. Ni marufuku kwa mtu yeyote:-

(a) Kuegesha chombo chochote katika sehemu ya kuegesha magari kinyume na utaratibu uliowekwa na Mamlaka.

(b) Kupakia au kuteremsha abiria yeyote au mzigo isipokuwa katika vituo vilivyowekwa kwa madhumuni hayo.

(c) Kupakia au kusababisha kupakiwa au kuteremsha mzigo au kuruhusu au kuteremshwa bidhaa kutoka katika gari isipokuwa katika kituo au sehemu iliyoainishwa na Mamlaka ya Serikali ya Mtaa au alama za barabarani zilizowekwa kisheria.

Scanned with CamScanner

(d) Kuegesha chombo chochote ndani ya masafa ya futi hamsini kutoka upande wa sehemu ya kuegesha ambapo alama imewekwa kisheria.

77.-(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuegesha chombo kinyume na utaratibu uliowekwa na Mamlaka au kutumia au kuondosha alama na vifaa vilivyoekwa kwa matumizi ya maegesho. Malipo ya kuegesha chombo na vifaa vya maegesho.

(2) Mtu yeyote atakaeegesha chombo kwa muda atalazimika kulipa ada ya uegeshaji kama itavyoelezwa katika Jadweli la Kanuni hizi na kama itakavyofanyiwa mapitio muda baada ya muda.

(3) Mamlaka ya Serikali za Mitaa itampatia mteja risiti ya malipo kwa huduma ya egesho ambayo itaonyeshwa kiwango cha ada ya huduma namuda wa chombo uliotumika katika egesho .

(4) Mamlaka au wakala alieidhinishwa na Mamlaka itahakikisha inaimarisha maeneo yote ya kuegesha vyombo kwa kutumia mistari iliyochorwa au zana nyenginezo kama itakavyoonekana inafaa, isipokuwa kwa kutokuwepo alama hizo hakutobadilisha malipo ya sehemu ya kuegesha vyombo.

(5) Mamlaka za Serikali za Mitaa au wakala inaweza kuanzisha sehemu maalum kwa ajili ya huduma ya kuegesha vyombo na malipo yake yataamuliwa na Mamlaka muda baada ya muda.

78.-(1) Mtu yeyote atakaekiacha chombo katika sehemu ya kuegesha vyombo ndani ya masaa ya udhibiti kwa kipindi kinachozidi wakati ulioruhusiwa, msimamizi wa mahali hapo atamtoza mmiliki wa chombo malipo ya kawaida na malipo ya ziada. Malipo ya kawaida na yale ya ziada.

(2) Malipo ya ziada kwa chombo kwa saa 1 au pungufu ya saa Shilingi elfu moja kwa saa (Tsh 1000).

79.-(1) Chombo kinaweza kuegeshwa katika sehemu ya kuegeshea vyombo nje ya saa za udhibiti bila ya malipo. Kuegesha chombo bila ya malipo.

(2) Mtu yeyote atakaeegesha chombo cha usafiri katika eneo la egesho na kupitiwa na muda wa udhibiti na kuingia muda mwengine wa udhibiti mmiliki atakuwa ametenda kosa na alalazimika kulipa faini za ziada pamoja na muda wa udhibiti kwa masaa yaliotumika kuegesha gari au chombo hicho.

80. Vyombo vifuatavyo vinaweza kuegeshwa katika sehemu za kuegesha vyombo ndani ya masaa ya udhibiti bila ya malipo:- Kusamehewa kufanya malipo.

(a) Vyombo vya usafiri wa Viongozi wenye hadhi ya ubalozi,

(b) Magari ya kuchukulia wagonjwa,

(c) Magari ya Serikali auMiradi ya Serikali ,

(d) Chombo cha usafiri kwa matukio ya dharura au Opereshenі ya uokozi.

(2) Mamlaka ya Serikali ya Mtaa haitokuwa na dhamana juu ya uharibifu wowote wa chombo cha moto,au gari au mali utakaotokea katika maeneo ya kuegesha magari.

Makosa.

**81.**-(1) Mtu yeyote atakeegesha gari au kulaza katika sehemu ya kuegesha au kulaza gari na:

(a) akakataa kulipa ada ya huduma ya maegesho au kulaza chombo cha moto;

(b) atakaegesha au kulaza gari zaidi ya muda alioruhusiwa kutokana na ada aliolipa;

(c) atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia ataozwa faini isiopungua shilingi 100,000/=na kuamrishwa kulipwa ada mara mbili ya zaidi ada iliyopo;

(2) Mtu yeyote :-

(a) atakaeweka kitu chochote chenye kuchukua nafasi katika eneo la egesho liliotengewakwa ajili ya maegeshoya magari au vyombo vya moto bila idhini ya baraza;

(b) atakaefanya shughuli yoyote inayoleta uchafuzi wa mazingira katika eneo la egesho la vyombo vya usafiri vya moto;

(c) atakaefanya shughuli za ufundi mekanika katika eneo la kuegesha magari;

(d) atakaeondosha alama au vifaa vya maegesho bila ya ruhusa.

atakuwa amefanya kosa na akipatikana na hatia atalazimika kulipa faini isiyopungua shilingiLaki mbili 200,000/na iasiozidi 300,000/=au kutumikia kifungo kisichopungua miezi mitatu, na kulipa gharama ya uharibifu wa vifaa vinavyotumika katika eneo la egesho la vyombo vya moto.

Adhabu.

**82.** Mtu yeyote anaenda kinyume na kanuni za sehemu hii atakuwa ametenda kosa na ikithibitika atalazimika kulipa faini isiyopungua shilingi laki tatu za kitanzania (Tsh 300,000/-) na isiyozidi Laki tano za kitanzania (Tsh 500,000/-) au atatumikia Chuo cha Mafunzo kwa muda wa wiki tatu au adhabu zote mbili.

Uwezo wa kuingia katika eneo.

**83.**-(1) Itakuwa halali kwa Mamlaka na Afisa wake, watumishi wake au mawakala wake kuingia katika eneo na jengo lolote katika wakati muafaka ili kufanya ukaguzi au uchunguzi au kutekeleza kazi yoyote ambayo Mamlaka imepewa uwezo wa kuifanya chini ya masharti ya kanuni hizi.

(2) Mtu yoyote atakaemzuia afisa yeyote aliyeidhinishwa katika utekelezaji wa kazi zake kwa mujibu wa masharti ya kanuni hii atakuwa mkosa kwa mujibu wa kifungu cha 82(1)(c) cha Sheria Nam. 7 ya 2014.

Scanned with CamScanner

84.-(1) Mtu yeyote atakaeshindwa kutii matakwa ya notisi yoyote iliyotumwa chini ya kanuni hizi ndani ya muda ulioanishwa katika notisi hiyo, atakuwa ni mkosa. Kushindwa kutii notisi/ indhari.

(2) Pale ambapo chini ya kanuni hizi, Mamlaka imepewa uwezo wa kutowa notisi kwa mtu yeyote ya kumtaka kuondosha au kukata mti wowote, au mmea wowote au kuvunja jengo, kuondosha, kujenga, kufanya kubadilisha au kukarabati jengo lolote, au kituo chochote, Mamlaka inaweza kwa notisi hiyo au notisi nyengine kumjuulisha mtu huyo kuwa ikiwa matakwa hayo hayakutimizwa. Mamlaka yenyewe itaingia katika sehemu husika ili kufanya kazi iliyoelekezwa katika notisi hiyo na pia jambo jengine lolote linaloweza kufanya kwa mujibu wa masharti ya notisi hiyo na gharama zote zilizojitokeza kwa kazi hiyo zitalipwa na mtu aliyeshindwa kutekeleza matakwa hayo.

85. Pale ambao notisi yoyote chini ya masharti ya kanuni hizi inahitajika kutumwa au kupewa mtu yoyote na Mamlaka, itatolewa kwa kupitia afisi yake, au makaazi ya kawaida ya mtu huyu, au wakala wake au kwa njia ya anuani ya posta ya mtu huyo au wakala wake, pale ambapo mtu huyo au wakala wake anayo afisi maalum, au maskani ya kudumu au sanduku la posta au pale anapokuwepo mashaka ya upatikanaji wa mtu huyo au wakala wake katika njia za kawaida zinazotumika, notisi itatolewa kwa kutumia taratibu zilizowekwa wa utumiaji notisi na amri za mahakama. Utumaji wa Notisi/ indhari.

86. Mtu yeyote atakaekiuka au kushindwa kutekeleza lolote katika masharti ya sehemu hii atakuwa ametenda kosa na atawajibika kulipa faini isiyopunguwa shilingi laki moja au kifungo kisichozidi mwezi mmoja au adhabu zote mbili kwa kosa la kwanza na ikiwa ataendelea kutenda kosa hilo atatozwa adhabu ya faini isiyopunguwa laki mbili au kifungo cha miezi miwili. Adhabu.

87.-(1) Kutakuwa na Jadweli la viwango vya malipo ya Huduma zinazotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Jadweli la malipo ya ada za huduma.

(2) Waziri anaweza kuongeza au kupunguza malipo ya ada za Huduma zinazotolewa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kama atakavyoona inafaa.

Scanned with CamScanner

## JADWELI NAMBA I

## MALIPO YA ADA KWA HUDUMA ZA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

Imeundwa chini ya kifungu namba 19(c),21(1),23(c),25(c), 26)(1)(b) /LESENI

| KIFUNGU | CHAZO CHA MAPATO | KIWANGO CHA ADA |
|---|---|---|
| UZALISHAJI | Vyeti vya mazao | 250,000/- Kwa jumla |
| FOMU | **AINA YA FOMU** | |
| | Leseni ya biashara | 10,000/- |
| | leseni ya Vileo/ nyumba za kulala wageni | 150, 000/- - 250,000/- |
| | Ujenzi | 20,000/- |
| LESENI | **AINA YA BIASHARA** | **KWA MWAKA** |
| | **VILEO:** | |
| | Hoteli yenye nyota 5 na 4 | 5,000,000/- |
| | Hoteli yenye nyota 3 na 2 | 4,000,000/- |
| | Hoteli yenye nyota 1 | 3,000,000/- |
| | Hoteli yenye nyota A, AA, AAA na chini ya kiwango | 2,000,000/- |
| | | |
| | **BIASHARA MADUKA:** | |
| | **Duka la chakula** | |
| | Jumla | 200,000 - 600,000/- |
| | Rejareja | 50,000 - 199,000/- |
| | **Duka la vinywaji** | |
| | Jumla | 150,000 - 500,000/- |
| | Rejareja | 80,000 - 149,000/- |
| | **Vifaa vya ujenzi** | |
| | Jumla | 300,000 - 600,000/- |
| | Rejareja | 150,000 - 299,000/- * |
| | **Viwanda** | |
| | Vikubwa | 500,000 - 3000,000/- |
| | Vidogo | 150,000 - 499,000/- |
| | **Duka la nguo/viatu** | |
| | Jumla | 250,000 - 600,000/- |
| | Rejareja | 80,000 - 249,000/- |
| | **Duka la vipodozi** ZFDA | |
| | Jumla | 300,000 - 500,000/- |
| | * Rejareja | 80,000 - 299,000/- |
| | Sonara | 150,000 - 600,000/- |
| | Maduka ya samani (funiture) | 150,000 - 600,000/- |
| | Yadi za magari | 300, 000 - 600,000/- |
| | Maduka ya nyama/samaki | 80,000 - 300,000/- |
| | Maduka ya gesi | 80,000 - 2,000,000/- |
| | * Maduka ya dawa ZFDA | 80,000 - 600,000/- |
| | vyakula vya mifugo/pembejeo | 80,000 - 300,000/- |
| | Maduka mchanganyiko | 80,000 - 300,000/- |
| | vifaa vy maofisini (stationary) | 80,000 - 500,000/- |
| | Fundi Ushoni | 80,000 - 300,000/- |
| | Huduma za Simu | 100,000 - 400,000/- |
| | Maduka ya Simu | 120,000 - 600,000/- |
| | Mikahawa | 100,000 - 600,000/- |
| | Huduma za Ofisi | 120,000 - 500,000/- |
| | Ghala | 300,000 - 1,000,000/- |
| | * Huduma za Mitandao (Internet Café) | 100,000 - 1,000,000/- |
| | Gereji | 150,000 -700,000/- |
| | Kuosha Vyombo vya Moto (Car Wash) | 100,000 - 700,000/- |
| | Kitalu | 80,000 - 200,000/- |
| | Vifaa chakavu (Used) | 100,000 - 1,000,000/- |
| | * Kampuni | 300,000 - 1,000,000/- |
| | ~~Vitu chakavu (Makachara)~~ | ~~100,000 - 600,000/-~~ |
| | Hall | 300,000 - 1,000,000/- |

1. Ukubwa na ada.
2. Viwango havieleweki
3. Viwango kutokana na Categories
4. Biashara na vibali vinavyosimamiwa na Sekta nyengine.

Scanned with CamScanner

| | | |
|---|---|---|
| | Maduka ya Toise | 150,000 - 600,000/- |
| | Benki | 1,000,000 - 2,000,000/- |
| | Beurede change | 500,000 - 1,000,000/- |
| | Bekari | 100,000 - 300,000/- |
| | Wakala wa usafirishaji (Clearing and forwarding) | 300,000 - 1,000,000/- |
| | Dobi (LAUNDRY SERVICES) | 150,000 - 1,000,000/- |
| | Saluni | 100,000 - 300,000/- |
| | Skuli binafsi | 100,000 - 1,000,000/- |
| | Hospitali binafsi | 200,000 - 2,000,000/- |
| | Maduka ya Madawa ya asili | 80,000 - 500,000/- |
| | Maduka ya Vitu vya Kitalii (Botique) | 80,000 - 700,000/- |
| | Maduka ya Viungo (Spice) | 100,000 - 500,000/- |
| | Vifaa vya Michezo | 100,000 - 500,000/- |
| | Vifaa vya Uvuvi | 80,000 - 500,000/- |
| | Mazao ya Baharini | 300,000 -1,000,000/- |
| | Nyumba za kulala wageni | 30,000 -150,000/- Chumba kwa Mwezi |
| | Vifaa vya Vyombo vya Moto (Auto spart) | 150,000 - 500,000/- |
| | Vifaa vya Baskeli | 80,000 - 200,000/- |
| | Waziba Mipira | 80,000 - 200,000/- |
| | Maduka ya Mbao | 250,000 - 600,000/- |
| | Duka la vyombo vya majumbani | 100,000 - 500,000/- |
| | Duka la miti | 150,000 - 700,000/- |
| | Sheli ndogo ya mafuta | 300,000 |
| | Sheli zinazoambatana na maduka | 3,000,000/- |
| | Sheli zisizoambatana na maduka | 1,500,000 - 2,000,000/- |
| BIASHARA NDOGONDOGO | AINA YA BIASHARA | KWA SIKU |
| | Vitafunwa | 200 - 1000/- |
| | Mbogamboga | 500 - 1000/- |
| | Matunda | 1000 - 3000/- |
| | Mazao (vyakula) | 500 - 2000/- |
| | Vinywaji | 500 -1000 /- |
| | Mazao ya misitu | 500 - 2000/- |
| | Mafundi | 1000 - 2000/- |
| | Mazao ya baharini | 2000/- |
| | Tanu moja ya makaa | 5000/- |
| | Tanu moja ya chokaa | 5000/- |
| | | |
| HUDUMA | VIBALI VYA UJENZI | |
| | Nyumba za kuishi | 50,000/- - 150,000/- |
| | Nyumba za kulala wageni | 200,000/-- 350000 |
| | Nyumba ya ghorofa | 1,000,000/- kwa ghorofa |
| | Ukuta (fensi) | 6500 kwa mita |
| | Minara ya simu | 5% ya gharama ya ujenzi |
| | Vituo vya mafuta | 500,000 - 1,000,000/- |
| | Mabwawa (swimming pool) | 1,000,000/- |
| | Shule | 500,000 - 1,500,000/- |
| | Dispensary | 500,000 - 1,500,000/- |
| | Mlango wa biashara | 50,000/ - 100,000/- |
| | Ghala | 500,000 - 1,000,000/- |
| | | |
| | USAFI | KWA MWEZI |
| | Vituo vya uuzaji wa mafuta (sheli) | 50,000 - 100,000/- |
| | Nyumba za kawaida | 3000/- |
| | Nyumba za plani | 3000/-- 5000/- |
| | Hoteli | 150,000 - 2,000,000/- |
| | Nyumba za kulala wageni | 50,000 - 100,000/- |
| | Duka | 6000 - 10,000/- |
| | Michirizi | 5.000 – 50.000/- |

Scanned with CamScanner

| | | |
|---|---|---|
| | Maji (taka) machafu | 250,000 - 300,000/- kwa trip |
| | Ghala | 50,000 – 100,000/- |
| | Ofisi binafsi | 25,000 – 50,000/- |
| | Genge | 500 - 1000/- kwa siku |
| | Mkahawa | 5000 - 10,000/- |
| | Muuza mitumba | 2000/- kwa siku |
| | Yadi za magari | 30,000 - 50,000/- |
| | Viwanda | 10,000 - 100,000/- |
| | Gereji | 10,000 - 50000/- |
| | Uchimbaji wa Mafuta | 5,000,000/- -- 10,000,000/- kwa mwaka |
| | HUDUMA NYENGINEZO: | KWA MWAKA |
| | Rout za magari ya abiria | 50,000/- |
| | Ukaguzi wa afya (nyumba za kulala wageni) | 50,000/- |
| | Ukaguzi wa afya (baa za kawaida) | 50,000/- |
| | Ukaguzi wa afya | 5000 - 10,000/- |
| | Maegesho ya magari | 1000/- kwa saa |
| | Ada ya kiingilio (entry fees) | 1000/- kwa siku |
| | Maegesho ya Vespa,Pikipiki na Honda | 500/-kwa saa |
| | Maegesho ya Baiskeli, mikokoteni na vinavyolingana navyo | 300/-Kwa saa |
| | Uingizaji wa mnyama ndani ya eneo la Mamlaka ya Serikali za mitaa | 10,000 Kwa mnyama. |
| | Machinjio | 5000 kwa mnyama |
| | Ada ya mikataba | 5% |
| | Beji ya udalali | 100,000/- kwa mwaka |
| | Ada ya udalali | 1000/- kwa siku |
| | Ada ya Bidhaa katika mnada | 2% ya bei ya bidhaa |
| | Mizigo ya biashara inayoingizwa katika maeneo ya Mamlaka | 5,000/- kwa gari kubwa |
| | Usafirishaji wa mazao ya baharini | 3000 - 10,000/- kwa gunia |
| | Usafirishaji wa mazao ya chakula | 3000 -10,000/- kwa gari |
| | Uratibu wa mazao ya bahari | 10,000 - 20,000 kwa mwezi |
| | Minara | 2,500,000 kwa mwaka |
| | Maonyesho / Matamasha | 5000- 10,000/- kwa siku |
| MICHEZO BAHARINI | AINA YA MICHEZO | ASILIMIA YA MAPATO YA MWEZI |
| | Vishada, | 10% |
| | Speed Boat | 10% |
| | Jahazi. | 5% |
| | Kima punju | 15% |
| | Dolfin | 5% |
| | Michezo mengine | 10% |
| | safari za kitalii visiwani na mafunguni | 1000-2000 kwa mtu |

**JADUELI NAMBA 2**
**USHURU WA USAFIRISHAJI WA MAZAO YA MISITU**

| | | |
|---|---|---|
| USAFIRISHAJI | AINA YA MAZAO | ADA YA MAZAO YA MISITU |
| | Kuni mzigo | 500/- |
| | Makaa polo au gunia moja | 500 - 1000/- |
| | Nguzo au miti | 2000/- kwa korija |
| | Fito | 500 - 1000/- kwa mzigo |
| | Asali debe au galoni moja | 2000/- |
| | Nta | 500/- kwa kilo |
| | usafirishaji mbao | 500/- kwa ubao |
| | Maliasili zisizorejesheka | 1500/- kwa tani moja |

Scanned with CamScanner

| | | |
|---|---|---|
| | Maliasili zisizorejesheka | 1000/- Chini ya tani moja |
| | Usafirishaji wa mazao | 1500 - 5000/- |
| | Usafirishaji wa Karafuu | 3000 - 5000 kwa gunia |
| | | |

**JADUELI NAMBA 3**
**MATANGAZO YA BIASHARA**

| AINA YA MATANGAZO | KIPIMO | ADA |
|---|---|---|
| Bango la kawaida | ft/sq | 15,000/- kwa mwaka |
| Mabango yanayojengewa kuta/mbao ngumu | | |
| Bango linalowaka taa | ft/sq | 20,000/- kwa mwaka |
| | ft/sq | 20,000/- kwa mwaka |
| Bango la TV | | 1,000,000 - 2,000,000/- kwa mwaka |
| Matangazo ya vitambaa | ft/sq | 30,000/- kwa wiki |
| Matangazo ya bomba kwa gari | | 50,000 - 100,000/- kwa siku |
| **Posters** | | |
| Karatasi nyepesi | 1-100 A4/ 1-50 A3 | 100,000/- Kwa mwezi |
| Karatasi nzito | 1-100 A4/ 1-50 A3 | 200,000/- Kwa mwezi |
| Vibati vya plastiki | 1-100 | 250,000/- Kwa mwezi |
| Maandishi/rangi kwenye ukuta | Mita | 15,000/- kwa mwaka |
| Michoro kwenye mabati (uzio)/paá | Mita sq | 15,000/- kwa mwaka |
| Michoro kwenye gari | Mita sq | 10,000/- kwa gari |
| Maonyesho ya kibiashara/ maeneo ya wazi | | 100,000/-kwa siku. |
| Maonesho ya kutumia gari/magari | | 50,000 - 100,000/- kwa siku. |
| sherehe ya kufunga njia za ndani | | 30,000/- Kwa siku |
| Gazebo | | 60,000/- kwa mwezi |
| Miamvuli/ meza | | 30,000/- kwa mwezi |
| mabango madogo | chini ya ft sq - 3 | 50,000/- kwa mwaka |
| mabango ya wakala | kwa moja | 100,000/- Kwa mwaka |
| Kubadilisha tangazo lililochakaa (bango) | | 50,000/- |
| Matangazo kwenye nguzo za taa/vibendera | kwa upande mmoja | 30,000/- kwa mwaka |

Imetiwa saini Leo tarehe 10 Mwezi 05 2017.

ZANZIBAR
Mei, 2017

(HAJI OMAR KHERI)
*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa Na Idara Maalum za SMZ Zanzibar.*

Scanned with CamScanner

# SHERIA YA TAWALA ZA MIKOA NAM. 8 YA 2014

## KANUNI ZA USULUHISHI WA MIGOGORO

## MPANGILIO WA KANUNI

KANUNI MAELEZO


SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI

1. Jina na kuanza kutumika
2. Matumizi.
3. Ufafanuzi.

SEHEMU YA PILI
UTARATIBU WA USULUHISHI MIGOGORO

4. Kupokea lalamiko la migogoro
5. Kutoa Wito.
6. Daftari la kumbukumbu za Migogoro.
7. Wajumbe wa Kamati ya usuluhishi migogoro.
8. Utaratibu wa Usuluhishi migogoro.
9. Maamuzi ya usuluhishi migogoro.
10. Kutofika kwa mlalamikiwa.
11. Kutofika kwa Mlalamikaji.

SEHEMU YA TATU
TAARIFA ZA KAMATI YA USULUHISHI MIGOGORO

12. Taarifa ya Maamuzi ya Kamati ya Usuluhishi Migogoro.
13. Kosa la kinidhamu.

SEHEMU YA NNE
HUDUMA ZA SHEHA

14. Huduma za Sheha.
15. Huduma bila Malipo.
16. Kosa la kutoza Malipo.


Scanned with CamScanner

## SHERIA YA TAWALA ZA MIKOA
## NAM. 8 YA 2014

---

## KANUNI ZA USULUHISHI WA MIGOGORO
**(Chini ya kifungu cha 33)**

---

**KWA UWEZO** niliopewa chini ya kifungu cha 33 cha Sheria ya Tawala Za Mikoa, Nam. 8 ya 2014, **Mimi HAJI OMAR KHERI** Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, natunga kanuni zifuatazo:-

### SEHEMU YA KWANZA
### JINA, KUANZA KUTUMIKA, MATUMIZI NA UFAFANUZI

1. Kanuni hizi zitajulikana kama kanuni za usuluhishi wa Migogoro ya mwaka 2017 na zitaanza kutumika mara tu baada ya kutiwa saini na Waziri husika. Jina na kuanza kutumika.

2. Kanuni hizi zitatumika katika Mikoa na Wilaya zote za Zanzibar Matumizi.

3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:- Ufafanuzi.

"Sheha" maana yake ni Kiongozi wa ngazi ya Shehia.

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Tawala Za Mikoa, Namba 8 ya mwaka 2014.

"Waziri" maana yake ni Waziri anayeshughulikia Tawala za Mikoa.

### SEHEMU YA PILI
### UTARATIBU WA USULUHISHI MIGOGORO

4.-(1) Mtu, Ukoo au kaya anaweza kupeleka lalamiko la mgogoro linalomkabili kwa Sheha au Katibu Shehia. Kupokea lalamiko la migogoro.

(2) Sheha au Katibu wa Shehia atapokea lalamiko lililowasilishwa kutoka kwa mlalamikaji na kuweka kumbukumbu katika daftari maalum la kumbukumbu za migogoro.

5.-(1) Mara baada ya Sheha kupokea lalamiko, Sheha atatoa barua ya wito kwa upande unaolalamikiwa kuhudhuria katika Ofisi ya Sheha si zaidi ya siku tatu. Kutoa Wito.

(2) Mlalamikiwa, baada ya kupokea wito wa Sheha, atalazimika haraka iwezekanavyo kufika katika Ofisi ya Sheha bila kuchelewa.

(3) Iwapo masaa 24 yamepita baada ya kuthibitika kufika kwa wito wa Sheha kwa mlalamikiwa na kushindwa kuhudhuria mbele ya Ofisi ya Sheha, mlalamikiwa atakuwa ametenda kosa na atalazimika kulipa faini ya Shilingi za Kitanzania elfu thalathini (30,000/-) itakayotumika katika uendeshaji wa shughuli za Ofisi ya Sheha.

(4) Katibu wa Sheha atalazimika kumpatia risiti Mlalamikiwa kuthibitisha malipo yaliyofanywa.

Daftari la kumbu-kumbu za Migogoro.

6.-(1) Kutakuwa na Daftari maalum la kuwekea kumbukumbu za Migogoro inayopelekwa, kusikilizwa na kusuluhishwa na Sheha katika Ofisi ya Sheha.

(2) Sheha kwa kushirikiana na Katibu wa Shehia, wataweka kumbukumbu za mambo yaliyoelezwa katika kanuni ndogo ya (1).

Wajumbe wa Kamati ya usuluhishi migogoro.

7.-(1) Kutakuwa na Kamati ya Usuluhishi Migogoro ambayo itaundwa na wajumbe wasiozidi watano watachaguliwa na Sheha kutoka miongoni mwa wajumbe wa Kamati ya Ushauri ya Shehia.

(2) Mwenyekiti wa Kamati ya Usuluhishi Migogoro atakuwa Sheha wa Shehia husika

(3) Katibu wa Kamati ya Usuluhishi Migogoro atakuwa Katibu wa Shehia ambae atakuwa hana uwezo wa kupiga kura.

Utaratibu wa Usuluhishi migogoro.

8.-(1) Bila ya kuathiri kifungu cha 18(2)(b) cha Sheria, katika kutekeleza kazi zake, Sheha kwa kushauriana na Kamati ya usuluhishi migogoro atafuata taratibu zifuatazo katika kusuluhisha migogoro inayowasilishwa katika Ofisi yake.

(2) Sheha, baada ya lalamiko kuwasilishwa kwake kwa mujibu wa taratibu zilizoelezwa katika kanuni hizi, ataanza kwa kuita majina matatu ya malalamikaji na kutaka aseme lalamiko lake mbele ya mlalamikiwa.

(3) Baada ya mlalamikaji kumaliza kusema, Sheha atampa fursa mlalamikiwa kujibu hoja zilizosemwa na mlalamikaji.

(4) Sheha anaweza kutoa fursa nyengine kwa mlalamikaji au mlalamikiwa, kumuuliza masuali au kujibu hoja zilizokuwa hazijajibiwa iwapo kutakuwa na haja ya kufanya hivyo.

(5) Ifahamike kwamba hakuna lalamiko litakaloamuliwa bila ya kuzikutanisha pande mbili za mlalamikaji na mlalamikiwa.

Maamuzi ya usuluhishi migogoro.

9.-(1) Sheha hatapaswa kufanya usuluhishi katika migogoro ifuatayo:

(i) mgogoro uliowahi kuwasilishwa Mahakamani na kutolewa uamuzi;

(ii) mgogoro iliokatazwa na kutolewa Tamko na Serikali

(iii) mgogoro uliokiuka sheria zilizopo Zanzibar.

(iv) mgogoro ulio katika makosa ya jinai

(2) Sheha kwa kushauriana na Wajumbe wa Kamati ya usuluhishi wa migogoro na baada ya kusikiliza vizuri pande zote mbili, atatoa uamuzi wa lalamiko lililowasilishwa mbele yake kwa mujibu wa taratibu zilizoelezwa katika kanuni na Sheria zilizopo Zanzibar.

Scanned with CamScanner

(3) Katibu wa Shehia ataweka kumbukumbu za lalamiko na maamuzi yaliyofikiwa katika daftari la usajili wa mgogoro.

(4) Iwapo imeshindikana kupata suluhu au upande mmoja haukuridhika na maamuzi ya Sheha, Sheha kwa maandishi, atamshauri mlalamikaji na mlalamikiwa kupeleka shauri lake katika vyombo vya Sheria.

(5) Maamuzi yaliyotolewa na Sheha kwa kushirikiana na Wajumbe wa Kamati ya Usuluhishi wa migogoro, yanaweza kutumika kama ushahidi Mahakamani.

10.-(1) Iwapo, baada ya wito wa kwanza kutolewa na mlalamikiwa kushindwa kufika katika Ofisi ya Sheha, Sheha atapanga siku nyengine ya kusikiliza lalamiko hilo. Kutofika kwa mlalami-kiwa.

(2) Iwapo mlalamikiwa atashindwa kufika katika Ofisi ya Sheha baada ya wito wa pili, Sheha atapanga siku nyengine na kumpelekea wito wa indhari ya kuamua lalamiko kwa kusikiliza upande mmoja.

(3) Iwapo Mlalamikiwa hakufika kwa mara ya tatu na bila ya kuwa na sababu ya msingi iliyowasilishwa kwa maandishi mbele ya Sheha, Sheha kwa kushauriana na Wajumbe wa Kamati ya Usuluhishi migogoro atatoa uamuzi kwa kusikiliza upande mmoja.

11. Iwapo malalamikaji, bila ya kuwa na sababu ya msingi iliyoandikwa, ameshindwa kufika katika Ofisi ya Sheha katika siku iliyopangwa, Sheha kwa kushauriana na Kamati ya Usuluhishi Migogoro atatoa uamuzi kwa kusikiliza upande mmoja na Katibu wa Sheha ataweka kumbukumbu ya Maamuzi yaliyofikiwa. Kutofika kwa Mlalamikaji.

## SEHEMU YA TATU
## TAARIFA ZA KAMATI YA USULUHISHI MIGOGORO

12.-(1) Kila Kamati ya Usuluhishi Migogoro kupitia Sheha wa Shehia husika italazimika kuwasilisha kwa Mkuu wa Wilaya taarifa ya malalamiko na maamuzi yaliyoamuliwa. Taarifa ya Maamuzi ya Kamati ya Usuluhishi Migogoro.

(2) Taarifa iliyoandaliwa na Kamati ya Usuluhishi Migogoro itawasilishwa katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ndani ya wiki mbili kutoka siku uliotoka uamuzi.

13. Iwapo Sheha, bila ya sababu ya msingi, atashindwa kuwasilisha taarifa kwa mujibu wa masharti ya Kanuni hizi, Mkuu wa Wilaya anaweza kumuwajibisha Sheha kinidhamu. Kosa la kinidhamu.

Scanned with CamScanner